

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

**SHULE YA SEKONDARI  
MASQARODA,  
S.L.P 234,  
KATESH – HANANG.**

.....

**Kumb. Na. MASQ/ADM/VOL.1/.....**

.....

**S.L.P 234 – MASQARODA,  
KATESH – HANANG.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASQARODA WILAYA  
YA HANANG MWAKA 2023**

Ninayofuraha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika **Shule ya Sekondari Masqaroda mwaka 2023**. Shule ya sekondari Masqaroda ipo umbali wa Km 32 kutoka Katesh makao Makuu ya Wilaya ya Hanang.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza kuanzia tarehe ..... na mwisho wa kuripoti ni tarehe

.....

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

***Sare za shule:***

Ni muhimu ifanane kwa rangi, mishono na ubora wake.

**WAVULANA:**

**Mwanafunzi aje na;-**

- ❖ Shati mbili nyeupe aina ya tetron mikono mifupi
- ❖ Suruali mbili rangi ya **Damu ya Mzee** (kitambaa aina ya namba moja) mishono wa kawaida marinda mawili.
- ❖ Sweta rangi ya Damu ya Mzee ifanane na rangi ya suruali - shingo V.
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi jozi moja vyenye kamba na visiwe na visigino virefu.
- ❖ Soski rangi ya khaki pea mbili.
- ❖ Mfuko wa madaftari/viatu
- ❖ T – Shirt (Fulana) yenye kola rangi ya Damu ya Mzee(zitapatikana shuleni)
- ❖ Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
- ❖ Mkanda wa suruali mweusi
- ❖ Truck suit ya dark blue kwaajili ya michezo.

**WASICHANA:**

- ❖ Blauzi (shati) mbili nyeupe aina ya tetroni mikoni mifupi
- ❖ Sketi ya rangi ya **Damu ya Mzee** (kitambaa aina ya namba moja),urefu wa sketi ukaribie kifundo cha mguu
- ❖ Sweta mbili zangi ya Damu ya Mzee ,ifanane na rangi ya sketi
  
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi 2
- ❖ Sweta rangi ya Damu ya Mzee ifanane na rangi ya sketi
- ❖ Soksi nyeupe stocking pair mbili
- ❖ Track suit ya dark blue kwa ajili ya michezo
- ❖ Mfuko wa vitabu au madaftari
- ❖ T-shirt (fulana) rangi ya Damu ya Mzee(zitapatikana shuleni)
- ❖ Kwa waisilamu, kitambaa cha kichwani kishuke hadi kifuani sketi ziwe ndefu zifunike kifundo cha mguu.

**MUHIMU:**

Rangi, mishono na aina ya nguo (material) ifanane na ya wanafunzi wengine kwa kitado cha kwanza kwa mujibu wa maelekezo.

**MAHITAJI YA SHULE:**

- a) Daftari kubwa (9) za masomo na zote ziwe counter book
- b) Vyombo vya chakula viwe vya aluminium (visiwe vya plastic) sahani, bakuli na kijiko
- c) Rula na kifuto (Raba) kwa matumizi yake kujifunzia
- d) Kamusi ya kiingereza ,nay a Kiswahili ya kujifunzia atakayotumia mwanafunzi mwenyewe.
- e) Mkebe wa hisabati.
- f) Fedha ya chakula, mlinzi na maji shilingi 52,000/= kwa mwaka ( 26,000/= kwa muhula zilipwe kwenye akaunti ya wazazi: **A/C NO 41010010409 :JINA LA AKAUNTI: KAMATI YA CHAKULA MASQARODA SECONDARI**, mahindi debe 3 kwa mwaka (debe 1 ½ kwa muhula) na maharag 1 ½ kwa mwaka (3/4 kwa muhula) viilipwe kwa mhasibu wa kamati ya wazazi ya chakula siku ya kuripoti shuleni

#### **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

#### **Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ya msingi;-**

##### **HESHIMA:**

- i. Wanafunzi wawe na heshima kwa walimu, wafanyakazi wote, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote anayewazidi umri.
- ii. Wanafunzi hawaruhusu kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe kwa wenyewe, kwa walimu na kwa mtu mwingine.
- iii. Wanafunzi wote ni lazima wahirikiane na kusaidiana na waheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
- iv. Wanafunzi wote hawaruhusiwei kufanya mambo yafuatayo;-
  - (a) Kuvuta sigara, bangi na kutumia madawa ya kulevya.
  - (b) Kunywa pombe
  - (c) kuvaa mavazi yasiyo na heshima
  - (d) Kugombana
- v. Wanafunzi wanatakiwa kuitika mara moja na kukimbia wanakoitwa
- vi. Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
- vii. Wanafunzi waheshimu kumbi za mikutano, ofisi za shule, kutunza na kuthamini mali binafsi na mali ya umma.
- viii. Wanafunzi wawe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote walipo
- ix. Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.
- x. Wanafunzi wanyooshe mkono juu na kusimama wanapouliza na kujibu maswali
- xi. Uhusiano kati ya mvulana na msichana uwe wa kimasomo tu.
- xii. Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
- xiii. Wanafunzi wote lazima wahudhurie kazi zote za mikono
- xiv. Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano yote ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi na kupandisha bendera ya Taifa.
- xv. Kwa kuzingatia sheria ndogo ya mahudhurio ya lazima katika shule ya sekondari Wilayani Hanang – mwanafunzi atakayekosa/acha shule **BILA SABABU YA MSINGI** pamona na **MZAZI/MLEZI** atakae sababisha mwanafunzi kuacha shule/masomo atachukuliwa hatua za **KISHERIA KWA KUZINGATIA SHERIA NDOGO HIYO.**

#### **A. KUWAHI:**

- i. Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa kwa ratiba ya kila siku, kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa zamu, kurudi shuleni baada likizo n.k

- ii. Wanafunzi ni lazima wawahi haraka wanaposikia wito wa dharura.

**B. UVAAJI WA SARE ZA SHULE:**

- i. Ni lazima mwanafunzi wote wavae sare ya shule wakati wote wa;-
  - a) Masomo ya darasani
  - b) Wanapotoka nje kwa shughuli za kishule
  - c) Mhadhara wa shule (Baraza)
  - d) Wanapokwenda hospitali
  - e) Maandamano rasmi
  - f) Wanapokuja shuleni na kurudi nyumbani jioni.
  - g) Kofia, kiatu cha ghorofa na mapambo yoyote haviruhusiwi kuvaliwa na asare
  - h) Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa kuvaliwa shuleni ni lazima uzingatiwe kwa kila hali.
  - i) Wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa buti nyeusi za mvua (Rainboots) wakati wa mvua. Usafi wa buti hizi ni muhimu kuzingatiwa.

**C. MIPAKA YA SHULE:**

- i. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali/ ruhusa maalumu na warudi kwa saa zilizoruhusiwa/pangwa.
- ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ya kibali maalumu;-
  - a) Ofisi za shule
  - b) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
  - c) Vilabu vya pombe
  - d) Vyumba vya starehe
  - e) Nyumba za kulala wageni

**D.MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI**

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na usagaji
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu makusudi mali ya uma
8. Kudharau bendera ya Taifa
9. Kuolewa au kuoia
10. Kupata mimba/ kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Wanafunzi kuwa na simu za mkononi

**E.MUHIMU (TANBIHI)**

Adhabu kwa uvunjaji wa sheria za shule zitatolewa na kamati ya nidhamu, baraza la walimu, Bodi ya shule na vyombo vingine vinavyohusika.Mzazi/mlezi anapaswa kumsimamia mwanafunzi katika masomo yake hasa anapokuwa nyumbani.

**KARIBU SHULENI MASQARODA**

.....  
**C B. MAGALI**  
**MKUU WA SHULE**

